## Maswali

1. Mbona Yakobo alienda Harani?
2. Raheli alikutana na Yakobo wapi?
3. Yakobo aliishi Harani kwa nani?
4. Binti wawili wa Labani ni nani?
5. Binti yupi alipendwa na Yakobo?
6. Yakobo alikubali kufanyia Labani kazi kwa miaka saba. Angepata nini baada ya hizo miaka saba?
7. Labani alimhadaa Yakobo namna gani? Mbona alimhadaa?
8. Ili amuoe Raheli pia, Yakobo alifaa afanye nini?
9. Yakobo alikuwa na wana wangapi?
10. Kutoka kwa wana wa Yakobo tunapata taifa gani?

## Majibu

1. Yakobo alienda Harani kwa sababu Esau alipanga kumua.
2. Yakobo alipata Raheli Harani kwa kisima.
3. Yakobo aliishi Harani kwa Labani.
4. Binti wawili wa Labani walikuwa Lea na Raheli.
5. Yakobo alipenda Raheli.
6. Mwisho wa miaka saba Yakobo angemuoa Raheli.
7. Labani alimhadaa Yakobo kwa kumpa Lea ili amuoe. Ilikuwa desturi yao binti mkubwa aolewe kwanza.
8. Alifanya kazi kwa miaka mingine saba ili amuoe Raheli.
9. Yakobo alikuwa na wana 12.
10. Wana 12 wa Yakobo ndilo taifa la Israeli.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 9 Yakobo anafanyia Labani kazi

**Kwa Biblia** Mwanzo 29: 1 – 30

### Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba Mungu alimwongoza na kumsaidia Yakobo. Yakobo alimdanganya Isaka babaye, sasa naye anadanganywa na Labani


### Somo

Esau alikasirika sana kwa sababu Yakobo alikuwa amepokea baraka kutoka kwa Isaka. Esau akapanga kumua Yakobo. Isaka na Rebeka wakamwambia Yakobo aende aishi na jamaa ya Rebeka huko Harani. Ataponea huko. Yakobo alipokuwa akienda Harani hakukuwa na furaha kuachana na Isaka na Rebeka.

Kulikuwa na hatari nyingi njiani. Alikuwa kwa hatari ya wanyan'ganyi pamoja na wanyama wakali. Lakini alifika Harani salama kwa sababu Mungu alikuwa naye.

Yakobo alifika Harani kwa kisima chenye Rebeka alikuwa amempa Eliezeri na ngamia maji. Yakobo alipofika kwa kisima, aliona wachungaji watatu na kundi la kondoo wao. Wachungaji walikuwa wanataka kupea kondoo wao maji kutoka kwa kisima. Yakobo aliwauliza kama wanamjua mjomba wake Labani [kakake Rebeka]. Kulikuwa na msichana akija na kundi la kondoo. Wachungaji wakamwambia, "Raheli ndio huyu, bintiye Labani."





Yakobo alifurahi kumwona binamu yake Raheli. Yakobo alikuwa amechoka kutokana na safari ndefu lakini aliwapa kondoo wa Raheli wote maji. Raheli alikimbia kuambia Labani kwamba mwana wa Rebeka alikuwa amekuja Harani. Labani alimkaribisha Yakobo akae nao.

Yakobo alikaa na Labani kwa mwezi moja na akaanza kumchungia kondoo. Kisha Labani alimuuliza Yakobo aseme mshahara atakaehitaji kwa hiyo kazi. Labani alikuwa na binti wawili - Lea na Raheli. Binti mdogo alikuwa mrembo na Yakobo alimpenda. Yakobo alimwambia Labani kwamba anataka amuoe Raheli. Akakubali kumfanyia Labani kazi kwa miaka saba ili amlipe mahari ya Raheli. Labani alifurahi na akakubali hayo mapatano. Yakobo naye alifurahi alipojua kwamba atamuoa Raheli baada ya miaka saba.

Kwa hiyo miaka saba Yakobo alifanya kazi kwa bidii. Alikuwa mchungaji mzuri. Miaka hiyo ilipita haraka kwa sababu alimpenda Raheli sana.

Miaka saba ilipoisha Yakobo alimwambia Labani kwamba anataka amuoe Raheli. Labani aliandaa karamu kubwa itakayomaliza juma moja. Yakobo alifurahi kwa kuwa Raheli atakuwa mke wake. Pamoja na rafiki zake walitazamia hilo juma la karamu.


Desturi ya nchi hiyo, binti mkubwa anaolewa kwanza. Labani alitaka Lea aolewe kabla ya Raheli. Labani hakumwambia Yakobo. Alimhadaa.



Labani alimvalisha Lea kama bi arusi. Ilikuwa desturi mwanamke kuweka utaji kwenye uso.Yakobo hangeona uso wa Lea. Alifikiria amemuoa Raheli. Yakobo hakukundua kwamba bi arusi ni Lea mpaka baada kuoana.

Yakobo alikasirika sana kwa kudanganywa. Alifanya kazi kwa bidii kwa miaka saba ili amuoe Raheli. Badala yake akamuoa Lea. Labani alikubali kwamba Yakobo angemuoa Raheli baada ya hilo juma la karamu. [Wakati huo wanaume walikubaliwa kuoa wake wengi]. Yakobo alikubali kufanya kazi tena kwa miaka saba ili alipe mahari ya kumuoa Raheli. Yakobo alikubali kufanya kazi tena kwa miaka saba kwa sababu alimpenda Raheli sana.

Yakobo alipokuwa akiishi Harani alipata wana kumi na wawili. Hawa wana wote walizaliwa na Lea na Raheli pamoja na wajakazi wao. Mungu alikuwa ameaahidi Ibrahimu kwamba atakuwa na taifa kubwa. Wana wa Yakobo kumi na wawili walikuwa makabila kumi na mbili. Makabila kumi na mbili hawa walikuwa taifa la Israeli. Mungu alikuwa anatumia maisha ya Yakobo kutimiza ahadi na baraka alizokuwa amepeana.




Baada ya miaka ishirini Yakobo alirudi kuishi kwa nchi ya Kanaani. Kwa somo lifwatalo tutajifunza vile alifanya amani na nduguye Esau na akaishi nchi ya Kanaani. Hii ni nchi yenye Mungu aliahidi atampa Ibrahimu na uzao wake milele.